

MAFUNZO YA TAALUMA MAALUM YA MATUMIZI SAHIHI NA SALAMA YA VIUATILIFU NA UDHIBITI WA VISUMBUFU TAREHE 6/5/2019 HADI 17/5/2019

UTANGULIZI

Matumizi ya viuatilifu katika kudhibiti visumbufu vya mimea na wadudu wanaoneza vimelea vya magonjwa ya wanyama na binadamu, yamekuwa yakiongezeka. Ongezeko hilo linatokana na kukua kwa shughuli za uzalishaji wa kilimo, ufugaji pamoja na ukuaji wa shughuli za kibiashara.

Matumizi ya viuatilifu ni muhimu sana na hivyo wazalishaji, wasambazaji, wauzaji, watumiaji, n.k wanapaswa kuwa na uelewa wa kutosha juu ya hifadhi, matumizi sahihi na salama ya viuatilifu na visumbufu. Viuatilifu visipotumiwa kwa usahihi madhara yake ni makubwa kwenye mazingira, afya ya wanyama, binadamu na mimea na zaidi havitaleta tija iliyokusudiwa katika kudhibiti visumbufu.

Ili kukidhi matakwa ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu, sheria na kanuni zimetungwa. Taasisi ya Utafiti wa viuatilifu kwenye ukanda wa kitropiki (*Tropical Pesticides Research Institute-TPRI*) imepewa jukumu la kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni hizo katika kufanya tafiti na kufikisha kwa wadau taarifa za kiutafiti kuhusu visumbufu, viuatilifu na shughuli zinazohusika. Hivyo basi TPRI hutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu na udhibiti wa visumbufu kila mwaka, mwezi Mei na Novemba.

MAFUNZO

Ili kutumia viuatilifu kwa manufaa na tija, ni muhimu kwa wadau wote wanaojihusisha na shughuli za viuatilifu kupata taarifa zinazohusu utaratibu wa uendeshaji wa shughuli hizo, taarifa za matumizi sahihi na salama ya viuatilifu, madhara ya viuatilifu kwa binadamu, wanyama, mimea na mazingira pamoja na udhibiti wa visumbufu. Mafunzo haya yameandaliwa kukidhi matakwa hayo. Mafunzo yanaendeshwa kwa nadharia na vitendo.

Kushirikiki kwenye mafunzo haya kutamwezesha mshiriki kupata uelewa sahihi juu ya usalama wa matumizi ya viuatilifu pamoja na udhibiti wa visumbufu, kujenga uelewa na mwelekeo wa kidunia kuhusu afya na usalama wa binadamu pamoja na biashara ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi n.k

WALENGWA WA MAFUNZO

Mafunzo haya yanawalenga wazalishaji, wasambazaji, wauzaji, watumiaji wa viuatilifu, wataalam wa kilimo na wakulima wadogo na wakubwa.

TATHMINI YA MAFUNZO

Washiriki wanatahiniwa, wanaofaulu hupewa Vyeti vinavyowapa sifa ya kufanya biashara za viuatilifu. Kwa mujibu wa sharia, kila mfanya biashara wa viuatilifu anapaswa kuwa na taaluma maalum ya viuatilifu inayotolewa na TPRI. Wataalam wa kilimo wanajengewa uwezo wa kuwahudumia wakulima katika maeneo yao kwa weledi zaidi.

MUDA WA MAFUNZO

Mafunzo yanaendeshwa kwa majuma mawili na yataanza tarehe 6/5/2019 hadi 17/5/2019 kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni. Kifungua kinywa, Chakula cha mchana na Usafiri wa kutoka na kurudi kwenye eneo la makazi jijini Arusha hutolewa. Makabrasha ya mafunzo ugawiwa kwa washiriki wote kwa ajili ya rejea.

MAHALI MAFUNZO YANAPOFANYIKA

Mafunzo yatafanyika TPRI makao makuu Ngaramtoni-Kibaoni Arusha, umbali wa Kilomita 12 toka katikati ya jiji la Arusha. Pia kila mshiriki atapata fursa za kutembelea na kujifunza kutoka kwenye maabara za TPRI.

MAWASILIANO

Mratibu wa Mafunzo-TPRI

Simu: 0272970464

Mob: 0759533420

Au: 0754272520

Barua pepe: dg@tpri.go.tz AU training@tpri.go.tz